



---

## MUKHTASARI WA SERIKALI YA KENYA KUHUSU MAUZO YA MIAKA MITATU YA KUPONI YA DHAMANA (M-AKIBA) INAYOTWAA UFADHILI KWA MUUNDO MSINGI

---



Save Money, **Make Money**, Build Kenya...

**TOLEO NAMBARI: MAB2/2017/3**

**THAMANI YA JUMLA: KSHS 1 BILIONI**

**JUNI 2017**

**IMETOLEWA KUPITIA KWA**

**SHIRIKA KUU LA HIFADHI YA HAZINA NA MASURUFU  
CENTRAL DEPOSITORY & SETTLEMENT CORPORATION (CDSC)**

**NA**

**SHIRIKA LA HISA LA NAIROBI  
NAIROBI SECURITIES EXCHANGE (NSE)**

Kwa maelezo kamili tafadhali tembelea  
Huduma Centre iliyo karibu au piga simu kwa **0206900020**  
(Tumebadili kutoka 0900889000)  
barua pepe **info@m-akiba.go.ke**  
au tembelea tovuti ya **www.m-akiba.go.ke**

## DHAMANA YA SERIKALI YA M-AKIBA NAMBARI MAB2/2017/3

Shirika kuu la Hifadhi ya Hazina na Masarifu, likiwa ndilo wakala wa Serikali ya Kenya wa M-AKIBA linawaalika wawekezaji wa rejareja ili kununua dhamana/bondi iliyotajwa hapa juu ambayo sheria na masharti yake ni kama yalivyoielezwa hapa chini:

Mtoa Mwaliko	: Serikali ya Kenya
Kiwango	: Kshs. 1 billioni (Yaweza kuongezwa hadi 3.85 billioni)
Lengo	: Ustawi wa Muundomsingi
Kipindi	: Miaka mitatu
Kuponi	: 10% kila mwaka
Mfumo wa Utumiaji	: Simu ya rununu kwa kubonyeza *889#
Tarehe ya kukadiria thamani	: 24/07/2017
Nukuu ya bei	: Par
Kiwango cha Chini	: Kshs. 3,000.00 (Kshs. 3000.00 Kiwango cha mwanzo kisha baadaye ziada yakurudia ya kshs. 500.00)
Kiwango cha Juu (mitandao za simu zinazoshiriki [MNOs])	: Kiwango cha Kshs. 140,000 kwa kila mwekezaji kila siku.
Kiwango cha Juu (Pesalink)	: Kiwango cha juu cha kwanza cha pesa ni Kshs. 999,999 kila mara unapotoa pesa; utoaji wa hela unaofuatia katika viwango vya mkupuo wa Kshs. 500 kwa siku.
Njia ya Malipo	: Mobile Money na PesaLink.
Tarehe za kulipa riba	: Kila baada ya miezi sita (kila mwaka) katika tarehe zifuatazo [22/01/2018, 23/07/2018, 21/01/2019, 22/07/2019, 20/01/2020, 20/07/2020]
Ushuru	: Mapato ya riba kutokana na M-Akiba hayatazwa ushuru
Tarehe ya malipo ya fidia	: 20/07/2020
Wakala wa kutoa na kulipa	: Shirika kuu la Hifadhi ya Hazina na Masurufu (CDSC)
Washirika wa kibiashara	: Madalali na Benki za Uwekezaji
Muda wa mauzo	: 30/06/2017 hadi 21/07/2017 au hadi jumla ya thamani ya dhamana itakapofikiwa, yoyote itakayotokea mwanzo
Mbinu ya ugawaji	: Mgao utatolewa kuambatana na nani atakayekuja mwanzo
Tarehe ya mwisho wa kutuma maombi	: Sharti maombi yawe yamepokelewa kufikia saa sita usiku, Julai 21, 2017
Uthibitisho wa Maombi	: Wawekezaji watapokea maelezo kuhusiana na kiwango walichowekeza kupitia ujumbe mfupi pindi tu baada ya kulipa kupitia kwa huduma ya malipo ya simu za rununu
Asilimia ya faida	: Washirika wa kibiashara watalipwa asilimia ya faida ya 0.1% ya mgao halisi
Orodha	: Dhamana hii itaorodheshwa kwenye Shirika la Soko la Hisa la Nairobi (NSE)
Mauzo ya pili	: Dhamana hiyo itauzwa kwenye NSE kupitia simu za rununu kuanzia Jumanne 25, Julai 2017
Uhalali	: Ni kwa watu waliojisajili kwenye huduma ya kutuma pesa kupitia mitandao za simu zinazoshiriki (MNOs) walio na walio na Kitambulisho cha Kitaiifa cha Kenya.
Mitandao za Simu Zinazoshiriki	: Airtel, Safaricom
Ufunguzi mpya	: Huenda ununuzi mpya wa dhamana ukafunguliwa katika tarehe ya baadaye
Haki ya kukubali maombi	: CDSC ina haki ya kukubali sehemu au maombi yote kwa jumla hadi kiwango kinachotarajiwa kitakapofikiwa